JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# HABARI NA MAWASILIANO

JARIDA LA MTANDAO

Toleo Na. 24, 2022 #KaziIendelee

# OPERESHENI ANWANI ZA MAKAZI 95%



TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

www.mawasiliano.go.tz Email: ps@mawasiliano.go.tz @wizarahmth

# MAPINDUZI YA KIDIJITI

Mapinduzi ya Kidijiti yameendelea kukua kwa kasi nchini Tanzania kufuatia dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa kwa jamii zinaendana na mabadiliko ya matumizi ya teknolojia Duniani. Matumizi hayo ya teknolojia yamechochea huduma za mawasiliano kuwa kiungo muhimu cha kuleta maendeleo kwa jamii kupitia nyanja mbalimbali za uchumi zikiwemo biashara mitandaoni, uwekezaji, elimu, habari, afya, sanaa, masuala ya ulinzi na usalama, n.k.

Jukumu hilo limekuwa likiratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo pamoja na majukumu mengine ya kisera, imekuwa ikihakikisha kuwa mawasiliano ya simu, data, redio na televisheni yanawafikia wananchi kwa wakati popote walipo nchini. Wizara pia inasimamia miradi mbalimbali ya miundombinu ya maendeleo katika sekta ya TEHAMA ambayo pia imehusisha ujenzi wa barabara ya mawasiliano kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano,.

Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaiweka Tanzania kuwa kiungo cha nchi majirani za Rwanda, Malawi, Burundi, Msumbiji, Kenya, Uganda, na Zambia ambapo mawasiliano baina ya jamii moja kwenda nyingine kupitia mifumo ya kidijiti yamekuwa yakisafiri masafa marefu na kumfikia mhusika kwa muda mfupi ambao ni rafiki na rahisi. Aidha, matumizi ya simu janja na kompyuta yamewezesha watumiaji kufanya mawasiliano ya ana kwa ana kwa maongezi ya faragha, kufanya mikutano, kufanya manunuzi au biashara mtandao, kutuma na kupokea pesa au kulipia ankara.

Mapinduzi ya Kidijiti yanadhihirisha jitihada kadhaaa za ushirikiano kati ya Serikali ya taasisi zake mbalimbali katika kuhakikisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki yanakuwa ni sehemu mojawapo ya kutoa huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu; huku Serikali inakusanya kodi na tozo mbalimbali kwa manufaa mapana ya Taifa. Ni matarajio ya Serikali kuwa uchumi wa Taifa utazidi kukua kupitia uchumi wa kidijiti ili kujikwamua na kuondokana na umaskini.




www.mawasiliano.go.tz Email: ps@mawasiliano.go.tz

@wizarahmth

Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 8.4 mwaka 2020. Ukuaji huu un athibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zinazotolewa na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara, mwaka 2021 asilimia 69 ya ardhi ya Tanzania inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani.

Aidha, takwimu za mwezi Aprili 2022, zinaonesha kuwa asilimia 95 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za simu za sauti na jumbe fupi, yaani 2G network kupitia minara 12,228. Asilimia 68 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za intaneti ya kasi ya 3G kupitia minara 11,753 na asilimia 45 wapo kwenye maeneo yenye mtandao wa 4G kupitia Minara 6,656.

Upatikanaji na utumiaji wa huduma ya intaneti ya 4G kwa wananchi wengi unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa kidigiti. Serikali ina dhamira ya kuweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma/ wawekezaji kujenga miundombinu ya mawasiliano ya intanenti ya kasi ili kuongeza wigo wa mitandao na kuimarisha ubora wa huduma za Mawasiliano ili kufikisha intaneti ya kasi kwa asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2025.

Mapinduzi ya kidijiti pia yamewezesha minara ya mawasiliano kujengwa katika kijiji cha Msomera, kilichopo Handeni, Mkoani Tanga, ambapo yanapatikana makazi mapya ya wananchi wa jamii ya wafugaji wanaohamia kwa hiyari kutoka katika hifadhi ya Ngorongoro. Mawasiliano ya simu yenye uwezo wa 4G na mawasiliano ya redio yamefikishwa kwa wananchi ili kurahisisha mahitaji yao ya kujenga Taifa.

Katika mazingira ya sasa ya kidijiti, huduma za mawasiliano zinawapatia wananchi fursa ya kujifunza nje ya elimu ya jadi kupitia simu janja, kompyuta na mtandao ambapo wanaweza kufanya utafiti na kujifunza. Vile vile, mawasiliano ya simu yamekuwa ni nyenzo muhimu katika suala la ulinzi na usalama, kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za uzalishaji pamoja na biashara.






# UTEKELEZAJI OPERESHENI ANWANI ZA MAKAZI SASA NI 95%

Zoezi la utekelezaji wa operseheni ya Mfumo wa Anwani za Makazi sasa umefikia asilimia 95 toka kutangazwa kwake na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Februari 8, 2022, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Conversion Centre uliopo jijini Dodoma. Mhe. Rais alielekeza kuwa utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ufanyike kwa njia ya Operesheni aliyoiita “Operesheni Anwani za Makazi” chini ya usimamizi wa Wakuu wa Mikoa na ukamilike ifikapo Mei, 2022.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (Mb) alieleza hayo wakati akikabidhi ripoti ya utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) tarehe 18 Juni 2022, katika Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

“Awali tulikuwa na lengo la kukusanya taarifa na kutoa Anwani za Makazi 11,582,106. Hata hivyo hadi tarehe 31 Mei 2022, tuliweza kukusanya taarifa na kutoa Anwani za Makazi 12,385,956 sawa na asilimia 106.94. Kati ya Anwani zilizokusanywa Anwani 12,011,576 zina majengo na 374,380 ni viwanja vitupu. Kati ya Anwani 12,011,576 zenye majengo, Anwani 2,011,095 ambazo ni asilimia 16.74 zimebandikwa vibao vya namba za nyumba na Anwani 5,738,552 ambazo ni asilimia 47.77 zimechorwa kwa rangi mithili ya vibao bila kubandikwa vibao,” alisema Waziri Nape.

“Operesheni hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya manufaa yaliyopatikana ni pamoja na kutoa Anwani 12,385,956 ndani ya miezi mitano (5) kazi ambayo awali ilipangwa kufanyika kwa

miaka mitano (5), Kuwa na Mfumo wa Kidijiti wenye taarifa muhimu za wananchi, majengo, viwanja na shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika majengo hayo pamoja na kutoa ajira za muda kwa vijana wakusanya taarifa 62,813 na wajasiliamali 8,667. Kwa ujumla utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi umefikia zaidi ya asilimia 95 na kwa sababu hiyo tunapata ujasiri," alieleza Waziri Nape.

Sambamba na hayo, Waziri Nape aliwapongeza viongozi na watumishi wa Wizara pamoja na wataalam wa mfumo wa kidigitali wa Anwani za Makazi ambao wameutengeneza na wamehakikisha unakuwa imara na unatumika wakati wote.

Mfumo wa Anwani za Makazi utakapokamilika utekelezaji wake utarahisisha uendeshwaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ifikapo Agosti 23, 2022 kwa kutambua kiurahisi watu na makazi wanayoishi.






# MSOMERA KUWA KIJIJI CHA KIDIJITI

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (Mb), amesema, zoezi la kuboresha huduma za Mawasiliano katika makazi mapya ya wafugaji wa jamaii ya Kimasai litawafanya waweze kupata taarifa mbalimbali duniani kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Waziri Nape amesema hayo wakati wa ziara ya ukaguzi wa upatikanaji wa huduma za Mawasiliano na ukusanyaji wa taarifa za Watu na Makazi katika kijiji cha Msomera kilichopo Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga ambako wakazi wapya kutoka Ngorongoro wanaishi.

“Mtakuwa na uwezo wa kuangalia Dunia kutokea Msomera hapa, na sisi kazi yetu ni kuwaunganisheni na Dunia ili mpate hizo huduma na ndiyo maana tumekuja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), tunataka watoto wenu waanze kujua kuchezea Kompyuta, wajue Dunia inavyoeenda na nina uhakika vijiji vingine vitawaonea wivu Msomera, ” alisema Waziri Nape.

Waziri Nape aliipongeza kampuni ya Airtel Tanzania kwa kupelekea huduma ya Mawasiliano katika kijiji hicho, pia mwisho wa mwezi huu mnara mkubwa unaojengwa na TTCL utakamilika na Wananchi wa kijiji hicho wataweza kupata huduma zote za Mawasilino kutoka mitandao yote nchini.

Sambamba na hayo Waziri Nape ameongeza kuwa Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ni jambo endelevu na hivyo aliongozana na wataalam wa Wizara yake ili kuhakikisha Msomera in-

Msomera kuwa Kijiji cha Kidijiti.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Siriel Mchembe ameipongeza kampuni ya Airtel Tanzania kwa kufanya kazi muda wote kufanikisha upatikanaji wa Mawasiliano katika kijiji hicho ambapo awali kulikuwa na shida ya mawasiliano.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msomera, Bw. Martin Olykei Paraketi alitoa pongez kufuatia juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha Msomera inakuwa na Mawasiliano bora pamoja na huduma nyingine za kijamii.

Serikali imekuwa ikitoa hamasa kwa jamii ya kabila ya Wamasai kuhama kwa hiari kutoka Ngorongoro na kwenda katika Kijiji cha Msomera kilichopo wilaya ya Handeni Mkoani Tanga, ili kutunza mazingira kwani jamii hii asili yao ni ufugaji na kwa miaka ya hivi karibuni imekuwa ikiongezeka kwa kasi na kuongezeka kwao pamoja na mifungo yao na hivyo kunahatarisha mazingira ya hifadhi ya Loliondo.





# WATU WENYE ULEMAVU LAZIMA WAHABARISHWE

Serikali imevitaka vyombo vya habari vya televisheni ambavyo bado havina wakalimani wa lugha za alama katika vipindi na ziara za viongozi wa kitaifa kuhakikisha wanatimiza sheria ya kuwepo wakalimani wa lugha hizo.

Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew (Mb) alisema hayo wakati akijibu swali la Mhe. Mbunge Khadija Taya kwenye kipindi cha maswali na majibu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Taya (Mb) alitaka kufahamu ni lini uwepo wa wakalimani wa lugha za alama kwa vipindi vya habari vya televisheni na ziara za viongozi utakuwa wa lazima.

"Nitoe wito kwa vituo vingine vya televisheni kufuata sheria na kuhakikisha wanawatumia wakalimani wa lugha za alama katika taarifa zao za habari na matukio mengine ya kitaifa ili kuhakikisha kwamba ndugu zetu wenye ulemavu wa kutosikia nao waweze kuhabarishwa," alieleza Mhandisi Kundo.

Sambamba na hilo, Naibu Waziri Kundo amesema mwaka 2018 sheria na kanuni ziliwekwa kwamba vyombo vya habari vinatakiwa kuwa na wakalimani wa lugha za alama na kwamba baadhi ya televisheni tayari zimetii sheria hiyo na ambavyo bado vinatakiwa kufanya hivyo.

Aidha, Mhandisi Kundo ameitaka mamlaka inayosimamia vyombo vya habari kuhakikisha wanawakumbusha wamiliki wa vyombo hivyo na wanaoratibu makongamano na matukio ya viongozi kuhakikisha wanatimiza wajibu huo kwa kuwa ni takwa la kisheria.




# WIZARA IKAWE MFANO FURSA ZA KIUCHUMI ZA SEKTA YA MAWASILIANO KITAIFA NA KIMATAIFA

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakusudia kuwa kitovu cha fursa katika Sekta ya TEHAMA Kitaifa na Kimataifa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Jim Yonazi alieleza hayo wakati akifungua kikao Kazi cha uchambuzi wa fursa za kiuchumi za Sekta ya Mawasiliano kitaifa na kimataifa jijini Dodoma leo. Dkt. Yonazi alisema kuwa kusudi la kikao kazi hicho ni kuangazia fursa za kisekta zilizopo nchini na mchango wake katika kukuza uchumi wa nchi. Serikali imelenga kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu fursa zilizopo katika sekta ya Habari, Mawasiliano na TEHAMA ili waweze kutumia vyema fursa zinazokuwa zinajitokeza ndani na nje ya Tanzania.

“Serikali imeweza kuweka mikakati ya kuwajengea uwezo watu pamoja na wadau ili kuhakikisha tunakuza sekta hii ya mawasiliano, kama mnavyo fahamu lazima tutekeleze mpango wa maendeleo kwa kuangalia yaliyomo ndani ya nchi yetu pamoja na mambo yanayoweza kuhamasisha,” alisema Dkt. Yonazi.


Dkt. Yonazi amesema Wizara hiyo ina jukumu la kuchambua na kuangalia ni nchi zipi Tanzania inaweza kushirikiana nazo, lakini pia kuangazia suala la ujenzi wa minara na kuongeza uwezo wa kutumia simu janja pamoja na usalama wa mtandao.

“Tunatakiwa kuwa Wizara ya mfano kwa kupanua wigo wa fursa za kiuchumi na kuandika historia

kwa kuifanya sekta ya mawasiliano kuchangia kwa kiwango kikubwa mabadiliko na mageuzi katika uchumi wa nchi yetu", alieleza Dkt. Yonazi. Lengo kubwa la kikao hiki ni kuiwezesha Tanzania kufikia malengo ya kukuza uchumi kupitia TEHAMA sambamba na fursa zingine zilizo kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Idara ya TEHAMA wa Wizara hiyo, Bw. Mulembwa Munaku alimuhakikishia Katibu Mkuu kuwa maelekezo yake yatatekelezwa na kuhakikisha kuwa mkakati unaandaliwa ili TEHAMA ichangie Pato la Taifa kwa asilimia 3% ifikapo 2025.





# HUDUMA ZA MAWASILIANO ZA ENDELEA KUBORESHWA MSOMERA

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake zimeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa jamii ya wafugaji wa kijiji cha Msomera kilichopo Handeni, Tanga. Wafugani hao ni wakaazi wapya waliohamia kwa hiyari katika kijiji hicho wakitokea katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

Kundi la nne la wananchi wanaohama katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro kwa hiyari kwenda katika kijiji cha Msomera, wilaya ya Handeni Mkoa wa Tanga lenye kaya 32 na jumla ya watu 188 na mifugo 880 limewasili na kupokelewa na Makatibu Wakuu wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Bw. Kaspar Mmuya, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Siriel Mchembe pamoja na wananchi, Julai 7, 2022.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Jim Yonazi alisema hayo wakati wa ziara ya Makatibu Wakuu katika kijiji cha Msomera iliyofanyika Julai 7, 2022 kwa madhumuni ya kukagua ujenzi wa miundombinu na ufikishaji wa huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi hao.

"Tutahakikisha upande wa mawasiliano hakuna changamoto tena katika kijiji hiki cha Msomera, tutaendelea kuratibu kadiri ambavyo wananchi wanaendelea kuongezeka katika kijiji hiki ili kila mmoja apate huduma bora za mawasiliano ya simu, redio, televisheni pamoja na Anwani ya Makazi ili waweze kushiriki katika uchumi wa kidijiti", alisisitiza Dkt. Yonazi.

Katibu Mkuu alieleza kuwa Wizara ina jukumu la kuwezesha na kuhakikisha jamii hiyo ya wafugaji wanakuwa na uwezo wa kupata na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili waweze kushiriki kikamilifu katika

kujenga uchumi wa nchi hasa uchumi wa kidijiti.

Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaendelea na uratibu kuhakikisha kunakuwa na maabara za kompyuta zenye vifaa vya TEHAMA (kompyuta, printa na projekta) katika shule ya msingi na sekondari zilizojengwa katika kijiji hicho ili kuboresha mazingira ya kufundishia na wanafunzi waweze kujifunza kisasa zaidi kupitia TEHAMA.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya Mifugo, Bw. Tixon Nzunda, ameipongeza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kufikisha huduma za mawasiliano katika kijiji hicho ambazo zinarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi waliohamia Msomera ambao asili yao ni wafugaji ambapo wataweza kupata vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yatokanayo na mifugo kwa njia ya mtandao kupitia simu ya mkononi au kompyuta kwa kuingia kwenye mfumo wa kielektroniki unaoitwa "Mifugo Integrated Management Information System" (MIMIS ).

Aidha, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Bi. Justina Mashiba amesema kuwa ujenzi wa mnara wa kudumu unaojengwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) katika kijiji cha Msomera unajengwa kwa ruzuku ya Serikali kupitia mfuko huo ambapo watoa huduma wengine wanaweza kupangisha kwa kuweka vifaa vyao na kuendelea kutoa huduma katika kijiji hicho.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mhandisi Peter Ulanga alisema kuwa ifikapo Julai 14, 2022, huduma za mawasiliano ya TTCL zitaanza kupatikana katika kijiji hicho lakini pia hadi mwishoni mwa mwezi Julai huduma za mawasiliano za kampuni za Tigo, Airtel, Halotel na Vodacom zitakuwa zinapatikana katika kijiji hicho ambapo wataweka vifaa vyao katika mnara huo.

Aliongeza kuwa ili kuhakikisha kunakuwa na mawasiliano ya uhakika katika kijiji hicho, TTCL itafikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika kijiji hicho ili kuhakikisha aina ya mawasiliano ya teknolojia ya 2G hadi 4G yanakuwa ya uhakika na kasi zaidi katika eneo lote la Msomera.

Mwenyekiti wa kijiji ncha Msomera, Bw. Martine Oleikai Paraketi aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuboresha sekta ya elimu kwa kuwezesha wanafunzi wa kijiji cha Msomera kujifunza kupitia vifaa vya TEHAMA na intaneti kuanzia shule ya msingi na Sekondari na wana imani kuwa Msomera itazalisha wasomi wengi.



# NAIBU KATIBU MKUU WHMTH AFANYA MAZUNGUMZO NA UJUMBE WA UMOJA WA ULAYA

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mohammed Khamis Abdulla kwa mara ya kwanza leo tarehe 18 Julai, 2022, amefanya ziara yake katika Makao Makuu ya Shirika la Posta Tanzania, jijini Dar es Salaam.

Lengo la ziara yake ni kuona namna Shirika la Posta linavyofanya shughuli zake katika kuwahudumia wananchi hususani katika eneo la usafirishaji wa barua, nyaraka, mizigo na vipeto. Aidha, Naibu Katibu Mkuu huyo amelipongeza Shirika la Posta Tanzania kwa kuendelea kuboresha huduma zake ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma stahiki na zenye ubora unaotakikana.

Katika hatua nyingine Bwana Abdulla alipata wasaa wa kutembelea Posta Kuu ya Dar es Salaam (GPO) na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Shirika hilo ikiwemo kutembelea kituo cha "Huduma Pamoja" kinachotoa huduma za Serikali kwa wananachi mahali pamoja zikiwemo zile zinazotolewa na NIDA, TRA, RITA, NHIF, PSSSF, BRELA na Uhamiaji, kilichopo katika ofisi hizo, jijini Dar es Salaam.





*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (Mb) akionyesha moja simu inayotumiwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Msomera, Martin Oleikayo Paraketi wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa huduma za Mawasiliano katika Kijiji hicho cha makazi mapya ya Wafugaji kilichopo Wilaya ya Hanadeni Mkoani Tanga.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Jim Yonazi akimpongeza Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Nape Nnauye (Mb) mara baada ya kukabidhi ripoti ya utekelezaji ya mfumo wa Anwani za Makazi kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim majaliwa Majaliwa katika ukumbi mikutano wa Kimataifa JICC, jijini Dar es Salaam.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Jim Yonazi (wa tatu kulia) akiwa na Makatibu wakuu wa Wizara mbalimbali na watumishi wao wakati wa ziara ya ukaguzi wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za kijamii katika makazi mapya ya Kijiji cha Wafugaji wa jamii ya Kimasai cha Msomera kilichopo Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga.*



*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (kulia), Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Anthony Mavunde (kushoto) wakikabidhi vifaa vya TEHAMA kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chinangali Juni 16,2022 jijini Dodoma.*

*Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,*
*Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*
*P.o. BOX 677, 40470 Dodoma, Tanzania*
*Email: ps@mawasiliano.go.tz*
*Website: www.mawasiliano.go.tz*
*Instagram: Wizarahmth*
*Twitter: Wizarahmtm*
*Facebook:Wizara hmth*